

## KUATHIRIANA KWA FONOLOJIA NA SINTAKSIA KATIKA LUGHA YA KISWAHILI

*Michael A. Mashauri*

*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam - Tanzania*

[mashauridar@gmail.com](mailto:mashauridar@gmail.com)

### **Ikisiri**

*Makala hii inaangalia jinsi mipaka ya kifonolojia katika kiwango cha nje ya neno inavyoathiriana na sintaksia katika kutoa maana ya tungo za Kiswahili. Inaziba pengo hili, ambalo halijafanyiwa kazi katika isimu ya Kiswahili, kwa kuonesha jinsi ambavyo usarufi na maana ya tungo za Kiswahili hutegemea uhusiano wa muundo wa kisintaksia na muundo arudhi wa tungo hiyo. Makala inaweka bayana kuwa kila tungo huwa na mipaka ya kifonolojia ndani mwake ambayo huweza kubadili muundo au aina ya tungo kisintaksia na hata kubadili maana iliyokusudiwa na msemaji ikiwa itabadilishwabadilishwa. Aidha, inaonesha jinsi maana iliyokusudiwa na msemaji au aina ya tungo iliyokusudiwa hubainishwa na utamkaji wa tungo husika. Data za utafiti huu zimekusanywa uwandani kwa kushuhudia mazungumzo mbalimbali ya watumiaji wa Kiswahili katika nyakati tofautitofauti na sehemu mbalimbali, matini mbalimbali na kwa njia ya mahojiano na watumiaji wa Kiswahili. Mkabala wa kinadharia uliotumika kuchanganua data ni ule wa Nadharia ya Muundo Arudhi. Matokeo yanaonesha kuwa kuna mwingiliano mkubwa baina ya fonolojia arudhi na sintaksia katika kufikisha ujumbe au maana ya tungo iliyokusudiwa.*

### **1.0 Utangulizi**

Mwingiliano wa vipashio vya kiisimu ni kipengele kimojawapo miongoni mwa vipengele muhimu katika kuelezea na kufafanua sarufi za lugha. Imekwishakuthibitika kwamba, matawi ya sarufi hufanya kazi kwa kuingiliana, kuathiriana na kushirikiana katika kuzalisha maumbo ya maneno na hata tungo kubwa zaidi ya neno zinazokubalika katika sarufi za lugha (Farmer, 1985; Ackema na Neeleman, 2004; Mashauri, 2018). Utafiti

huu unabainisha jinsi taarifa za kisintaksia zinavyoingizwa katika matamshi na jinsi matamshi yanavyoweza kuamriwa na muundo wa sintaksia wa tungo za Kiswahili katika mchakato wa kutoa ujumbe uliokusudiwa. Utafiti unaohusu kuingiliana kwa nyanja hizi huzingatia kuonesha muundo arudhi na muundo wa kisintaksia na jinsi miundo hiyo inavyoingiliana katika kutoa taarifa iliyokusudiwa. Utafiti unaohusu kuathiriana kwa fonolojia na sintaksia hufanyika kwa kuhusisha vipengele arudhi vya tungo ambavyo hupangiliwa kimsonge kwa kuanza na tamko, kirai-kiimbo (kirai cha kiimbo), kirai-fonolojia (kirai cha kifonolojia – ngazi ya kati ya kiarudhi) na neno-fonolojia (neni linalotamkika), bila kuhusisha egemeo-mkazo na silabi (Selkirk, 1978/1981; Truckenbrodt, 1995).

Kwa mfano:

Baba mdogo anawapenda wana wake	(Tamko/tungo)
$\Phi$  Baba mdogo anawapenda wana wake  $\Phi$	(Kirai-kiimbo)
(Baba mdogo) $\varphi$ (anawapenda wana wake) $\varphi$	(Kirai-fonolojia)
$\omega$ {Baba} $\omega$ {mdogo} $\omega$ {anawapenda} $\omega$ {wana} $\omega$ {wake} $\omega$	(Neno-arudhi)
$\$Ba\$ \$ba\$ \$m\$ \$do\$ \$go\$ \$a\$ \$na\$ \$wa\$ \$pe\$ \$nda\$ \$wa\$ \$na\$ \$wa\$ \$ke\$ \sigma$	(Silabi)

Maneno katika tungo huwa yamepangwa kwa kanuni za kisintaksia na hutawaliwa na kanuni na sheria mahususi za mshikano na mfuatano wa maneno hayo. Kila namna ya mshikano fulani wa maneno unaounda kipashio fulani, kama vile kirai, kishazi au sentensi, huwa na mawanda yake kisintaksia na kimatamshi pia (Elfner, 2018). Kwa upande wa fonolojia, mawanda hayo yanaanzia katika ngazi ya sauti, silabi, egemeo-mkazo, neno-fonolojia, kirai fonolojia, kirai-kiimbo na tamko zima ambayo hubainishwa kwa kiimbo, wakaa na toni katika lugha (Selkirk, 1978; Buring, 2016). Katika sintaksia, mawanda hayo huwa ni neno, kirai, kishazi au sentensi ambayo huthibitishwa kwa majaribio mbalimbali.

Kuna mielekeo miwili katika uchanganuzi wa uhusiano wa fonolojia na sintaksia kupitia muundo arudhi (Selkirk, 1978). Mwelekeo wa kwanza ni ule unaodai kuwa kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya muundo arudhi wa tungo na muundo wa kisintaksia na kwamba muundo wa kisintaksia ndio hutawala muundo arudhi na kuamua maana ya tungo. Mwelekeo huu unadai kuwa pale palipo na mpaka wa muundo fulani wa kisintaksia, basi pana mpaka pia wa muundo wa kiarudhi. Mwelekeo wa pili unadai kuwa hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya muundo wa kisintaksia na muundo wa kiarudhi na kwamba muundo arudhi huweza kuathiri pia muundo wa kisintaksia (Elfner, 2016). Aidha, kuna mikabala na vipengele kadhaa kuhusiana na mwingiliano wa sintaksia na fonolojia arudhi. Makala hii inaonesha ule uhusiano wa mpangilio wa vipengele vya kiarudhi na ule wa vipashio vya kisintaksia katika kutoa ujumbe unaokusudiwa. Kuna miundo inaonesha uhusiano wa moja kwa moja kati ya vipashio vya kisintaksia na ile ya kiarudhi na miundo mingine inaonesha kutotangamana. Aidha, imebainishwa pia kuwa, katika baadhi ya tungo, ikiwa mawanda ya kimatamshi yanapunguzwa au kupanuliwa, maana ya tungo pia hubadilika na vipashio vya kisintaksia. Katika kudhihirisha ujitokezaji huo, na kwa ajili ya kurahisisha uelewa juu ya utokezaji wa maathiriano haya, tumetumia tungo ambazo mabadiliko yake ya maana hutokana na utamkaji tofautitofauti.

Utafiti huu ni muhimu kwani unaongeza maarifa katika isimu ya Kiswahili ambayo bado hayajawekwa bayana na wataalamu wa isimu ya Kiswahili. Pengo hili ni muhimu lizibwe kwani kumekuwa na changamoto hata kwa waandishi wanaotumia Kiswahili katika kuandika tungo sahihi kutokana na kutoelewa jinsi utamkaji unavyofanya kazi pamoja na sintaksia. Mathalani, baadhi ya waandishi huweka koma (inayowakilisha mpaka wa kifonolojia) mahali ambapo hapastahili kisintaksia kwa sababu tu wanausikia mpaka huo katika utamkaji. Wengine wanashindwa kuuweka mpaka huo panapostahili kwa kushindwa kuelewa jinsi mipaka hiyo ya fonolojia-arudhi inavyochangia kutoa maana iliyokusudiwa katika tungo husika. Kwa mfano, baadhi ya waandishi huandika, *Mwalimu alisema kwamba, atakuja leo*; koma hii imewekwa kimakosa kutokana na kuisikia katika matamshi.

Wengine huandika, *Mwalimu alisema, kwamba atakuja leo*. Koma iliyotumika katika tungo hii haikuwa mahali sahihi kimatamshi ingawa kisintaksia imekigawa kwa usahihi kipashio tegemezi kinachoanza na ‘kwamba’. Mambo kama haya yanatokana na kukosekana kwa maarifa ya mipaka ya fonolojia-arudhi na uhusiano wake na muundo wa tungo katika kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Hivyo, makala, kwa sehemu, inatoa msaada kwa wanaisimu na hata waandishi kuwa na msingi wa maarifa ya uhusiano wa vipengele hivi.

## 2.0 Nadharia

Makala hii iliongozwa na Nadharia ya Muundo Arudhi ambayo mawazo yake yalianza katika kazi za Selkirk (1978) na kuendelezwa na wataalamu wengine kama Nespor na Vogel (1982, 1986). Nadharia hii inadai kuwa katika muundo wa kisintaksia kuna muundo arudhi pia. Kwa kuwa kuna pande mbili, tunaweza kusema kuwa mpangilio wa sentensi kiarudhi una muundo wa kimsonge wa vipengele arudhi ambao ni tofauti na ule wa kisintaksia na hutawaliwa na mashartizuizi yake ya ukubalifu wa muundo arudhi au huweza kuwa sawa na ule wa kisintaksia. Muundo arudhi ni sehemu ya sarufi ya lugha na hufanya kazi ya kuunganisha muundo wa kisintaksia na fonetiki (umbo la nje) wa tungo (jinsi tungo inavyotamkwa (Elfner, 2016). Nadharia hii inazingatia mpangilio msonge wa vipengele vya kiarudhi kulingana na ukubwa wake, ambao ni mpangilio wa kimajumui wa muundo arudhi (Selkirk, 1978). Hivyo, uchanganuzi wa nadharia unazingatia mgawanyo wa tungo kiarudhi kuanzia silabi ( $\sigma$ ), egemeo mkazo ( $\Sigma$ ), neno-arudhi ( $\omega$ ), kirai-fonolojia ( $\varphi$ ), kirai-kiimbo ( $\Phi$ ) na tungo/tamko. Katika makala hii, umeoneshwa ujitokezaji wa miundo hiyo na jinsi inavyoathiriana katika kutoa ujumbe uliokusudiwa.

## 3.0 Methodolojia ya Utafiti

Kila utafiti hufanyika kwa mbinu zilizo bayana na zinazofaa kwa utafiti husika. Makala hii ni matokeo ya utafiti wa kitaamuli uliofanyikia uwandani, mkoani Dar es Salaam, Wilaya ya Ubungo, ambako data



zilikusanywa kwa mbinu ya ushuhudiaji, mahojiano na usomaji matini. Mtafiti, katika nyakati tofautitofauti, alishuhudia mazungumzo mbalimbali ya watumiaji wa Kiswahili na kukusanya data ya namna wanavyoweka mipaka ya kifonolojia katika tungo wanazozitamka na kuhoji maana wanazozikusudia. Makundi ya mazungumzo yaliyotumika ni yale ya wanafunzi darasani na katika mazungumzo ya walimu kwa walimu maofisini. Wanafunzi na walimu waliohusishwa ni wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam. Aidha, mtafiti alikusanya tungo kadhaa kutoka katika matini mbalimbali na kuwataka watumiaji wa Kiswahili wazitamke huku wakieleza maana wanazozikusudia kulingana na mipaka ya kifonolojia-arudhi inayojibainisha katika utamkaji wao. Watoa taarifa hao walisampulishwa kwa usampulishaji kutegemea fursa. Matini zilizotumika katika kupata data ni kazi mbalimbali za wanafunzi zilizowasilishwa katika mijadala ya semina.

#### **4.0 Uwasilishaji na Uchambuzi wa Data**

Kimsingi, utamkaji wa sentensi huwa na midhihiriko ya vipandevipande vya kimatamshi. Vipande hivi huoneshwa kwa kutumia mipaka/kingo za kiarudhi na hudhihirika kulingana na taarifa inayotolewa. Utamkaji mbaya wa vipande hivyo, ambavyo huwa katika mawanda arudhi yake, huweza kusababisha utamkaji mbaya wa tungo unaopotosha maana au kuleta maana ambayo haikukusudiwa na msemaji. Mipaka mikubwa inaweza kubainishwa kwa wazi zaidi, hasa ile ya kirai-fonolojia na karai-kiimbo ilhali ule wa neno fonolojia unaweza usisikike bayana, hususani msemaji akiwa anakusudia kutoa ujumbe unaotolewa na kirai au kishazi kizima. Hata hivyo, mipaka hiyo inaweza kubainishwa na athari zake kimaana zinakuwa wazi endapo utamkaji hautazingatia mipaka yake. Uchanganuzi wa data katika makala hii unatumia mkabala unaozingatia mipaka ya kisintaksia na kiarudhi. Hivyo, uchanganuzi unaonesha jinsi utamkaji unavyoizingatia mipaka hiyo ya kiarudhi na ya kisintaksia na inavyoathiriana katika kutoa au kuathiri maana inayokusudiwa.

Katika Kiswahili kuna tungo ambazo utamkaji hauoneshi tofauti za wazi baina yake ingawa zina hadhi tofauti kisintaksia. Utamkaji huunganisha vipashio viwili vya kisintaksia kana kwamba ni kipashio kimoja cha kifonolojia. Hivyo, utamkaji wa kirai-fonolojia unaendana na utamkaji wa neno-fonolojia. Tazama mifano hapa chini iliyokusanywa katika ushuhudiaji wa mazungumzo ya wanafunzi darasani:

1. Tuna hofu vs Tunahofu



**Chanzo:** Uwandani (2022)

Pamoja na mipaka hii kuwa bayana kimaandishi, utamkaji wa tungo kama hizi katika Kiswahili hauoneshi mipaka ya wazi kama ilivyo katika maandishi. Tungo hizi zinakuwa na tofauti ya wazi ikiwa zitaingizwa katika kirai-kiimbo.

2. (a)  $|((\{Tuna\}\omega \{hofu\}\omega \{kubwa\}\omega)\phi ((\{ya\}\omega \{kutokea\}\omega \{kwa\}\omega \{njaa\}\omega)\phi | \Phi$   
 $|((\{Tunahofu\}\omega \{kwamba\}\omega)\phi ((\{yatokea\}\omega \{mabaya\}\omega)\phi | \Phi$
- (b)  $|((\{Una\}\omega \{hitaji\}\omega \{gani\}\omega)\phi ((\{linalokusumbua?\}\omega)\phi | \Phi$   
 $|((\{Unahitaji\}\omega \{nini\}\omega)\phi ((\{nikupatie?\}\omega)\phi | \Phi$

**Chanzo:** Uwandani (2022)

Sentensi ya 2 (a) na (b) zinaonesha tungo hizo mbili (*Tuna hofu* na *Tunahofu*) kwamba ni tofauti kisintaksia kulingana na maana inayotolewa. Kifonolojia, tofauti yake si bayana katika msikiko; hivyo, mzungumzaji asipoupanua muundo wa kisintaksia, msikilizaji anaweza kupata changamoto kuipata maana iliyokusudiwa kwa kusikia tu (labda kama atahusisha na muktadha wa mazungumzo). Hali hiyo hujitokeza pia katika tungo kama vile *Una hitaji* na *Unahitaji* au *wana wake* na *wanawake*. Hali hii inaonesha namna viwango hivi vya sarufi huingiliana katika kutoa ujumbe uliokusudiwa na msemaji.

Kuna tungo nyingine za aina hii ambazo hutofautishwa kimaana na sifa nyingine za kiarudhi na si mipaka ya kifonolojia au kisintaksia. Data hapa chini kutoka katika mahojiano ya wanafunzi wa Kiswahili inaonyesha mifano hiyo:

3. (a) Tuna tupa vs Tunatupa  
 (({tuna}ωT {{[tu:pa]}ω})φ      {tunatupa}ω
- ```

graph TD
    phi((φ)) --- omega1((ω))
    phi --- omega2((ω))
    omega1 --- Tuna
    omega2 --- tupa
            
```

```

graph TD
    omega((ω)) --- Tunatupa
            
```
- (b) Wana meza vs Wanameza  
 (({wana}ωT {{[mɛ:za]}ω})φ      {wanameza}ω
- ```

graph TD
    phi((φ)) --- omega1((ω))
    phi --- omega2((ω))
    omega1 --- Wana
    omega2 --- meza
            
```

```

graph TD
    omega((ω)) --- Wanameza
            
```
- Chanzo:** Uwandani (2022)

Mipaka ya kifonolojia katika tungo hizi ipo bayana ambapo inabainika kimsikiko waziwazi kutokana na neno la pili katika kirai fonolojia kuwa na wakaa mrefu. Hivyo, tofauti ya maana za tungo hizi hutegemea kingo za

kifonolojia ambazo hubainishwa na wakaa katika utamkaji. Hali hii inaelezwa pia na Downing (2013) anayedai kuwa, katika lugha zenye kirai-fonolojia changamani, viwango vya kiarudhi vinavyoathiri maana ya tungo si tu neno-fonolojia, kirai-fonolojia au kirai-kiimbo bali huhusisha viwango vingine vya kiarudhi. Katika kazi hiyo, amezungumzia toni katika lugha kama Kitsonga ambapo toni huhusika pia katika kuonesha uhusiano wa fonolojia na sintaksia.

Tungo nyingine zina mipaka ya kiarudhi ambayo ipo bayana kabisa kimatamshi na kimaana na huendana na kategoria za kisintaksia ingawa uandishi una changamoto. Tungo hizi ni kama katika data ifuatayo hapa chini kutoka katika kazi za wanafunzi na mahojiano:

4. (a) Anapenda sana kutoka kwao vs Anapenda sana kutoka kwao  
|({Anapenda}ω {sana}ω)φ {kutoka}ω {kwao}ω)φ | Φ  
(Anapenda sana kufika mahali akitokea nyumbani kwao)  
|({Anapenda}ω {sana}ω)φ {kutoka kwao}ω | Φ  
(Anapenda sana namna walivyotoka)
- (b) Anahitaji chakula cha kula vs Anahitaji chakula chakula  
|({Anahitaji}ω {chakula}ω)φ ({cha}ω {kula}ω)φ | Φ  
(Anahitaji apate chakula ili ale)  
  
|({Anahitaji}ω {chakula chakula}ω)φ | Φ  
(Anahitaji kitu ambacho kiko kama chakula)
- (c) Baba mdogo mdogo  
|({baba}ω {mdogo}ω {mdogo}ω)φ | Φ  
(Mdogo wake na baba ambaye ni mdogo zaidi ya wadogo zake wengine na baba)  
  
Baba mdogo mdogo  
|({baba}ω {mdogomdogo}ω)φ | Φ  
(Baba fulani ambaye ana umbo dogo/mwenye umri mdogo)



**Chanzo:** Uwandani (2022)

Maana ya tungo ya 4 (a), (b) na (c) hapo juu hutegemea namna utamkaji unavyojitokeza katika tungo hizo. Ikiwa zitatamkwa bila kuzingatia mipaka ya kifonolojia basi maana za tungo hizo huweza kutoeleweka kama anavyokusudia msemaji. Aidha, aina ya kipashio cha kisintaksia kinachokusudiwa kutolewa na msemaji huamua ujitokezaji wa mipaka ya kiarudhi katika tungo hizo. Mathalani, ikiwa msemaji wa tungo 4 (a) anakusudia kusema ‘kutoka kwao’ iwe ni kitenzi jina, basi lazima fonolojia italazimishwa kuvunja mpaka wa neno fonolojia kati ya ‘kutoka’ na ‘kwao’ ili kuwa na utamkaji wa kama neno moja. Pia, kutakuwa na kuushusha hadhi muundo arudhi huo kutoka kuwa kirai-fonolojia kuwa neno-fonolojia kama uchanganuzi unavyoonesha hapo juu. Tungo ya 4 (b) na (c) nayo inafuata utaratibu huohuo. Hivyo, utamkaji unaweza kuathiri muundo wa kipashio cha kisintaksia na kinyume chake kulingana na mahitaji ya msemaji au ya kimuundo. Hali kama hii hujitokeza pia katika lugha mbalimbali duniani kama inavyobainishwa na Elfner (2018).

Mifano mingine ya udhihirikaji wa mipaka ya kiarudhi na maathiriano yake na sintaksia hujitokeza katika maneno kama vile *vilevile*, *mbali*, *mbalimbali*, na kadhalika. Mifano ya tungo hapa chini inadhihirisha ujitokezaji huo kwa mujibu wa mahojiano na wasemaji na wataalamu wa Kiswahili:

5. (a) Alipanga vitabu vile vile. vs Alipanga vitabu vilevile.

$$|(\{Alipanga\} \omega \{vitabu\}) \phi (\{vile\} \omega \{vile\}) \phi | \Phi$$

(Hakupanga vitabu tofauti na vya awamu ya kwanza)

$$|(\{Alipanga\} \omega \{vitabu\} \omega \{vilevile\}) \phi | \Phi$$

(Alipanga vitu mbalimbali na vitabu pia)

- (b) Alipanga vitabu mbali mbali. vs Alipanga vitabu mbalimbali.

$$|(\{Alipanga\} \omega \{vitabu\}) \phi (\{mbali\} \omega \{mbali\}) \phi | \Phi$$

- (i) (Alipanga vitu kwa kuacha nafasi kati ya kimoja na kingine)

$$|(\{Alipanga\} \omega \{vitabu\} \omega \{mbalimbali\}) \phi | \Phi$$

(ii) (Alipanga vitu vya aina anuwai)

(c) Panga vitabu sawa sawa vs Panga vitabu sawasawa.

$|(\{Panga\}\omega\{vitabu\}\omega)\varphi(\{sawa\}\omega\{sawa\}\omega)\varphi|\Phi$

(i) (vitabu vipangwe kwa ulinganifu fulani kama vile wa idadi, na kadhalika)

$|(\{Panga\}\omega\{vitabu\}\omega\{sawasawa\}\omega)\varphi|\Phi$

(ii) (Panga vitabu kama vinavyotakiwa kupangwa)

**Chanzo:** Uwandani (2022)

Mifano 5 (a) – (c) hapo juu inazidi kuonesha namna utamkaji wa tungo unaathiriana na sintaksia katika kutoa ujumbe unaokusudiwa na msemaji. Ikiwa msemaji anakusudia kutoa maana (i) halafu akafuta mpaka wa neno-fonolojia kati ya maneno *vile* na *vile*; *mbali* na *mbali*; na *sawa* na *sawa* katika utamkaji wake, basi msikilizaji wake atapokea maana ya (ii) na kuathiri mawasiliano.

Miundo mingine inayodhihirisha maathiriano ya fonolojia na sintaksia kupitia uarudhi ni ile inayotumia vitenzi vishirikishi vya a-unganifu. Mifano ifuatayo kutoka katika mazungumzo ya wanafunzi darasani inadhihirisha ujitokezaji huo:

6. Majibu ya katika kitabu chao vs Majibu ya katika kitabu chao

$|(\{Majibu\}\omega\{ya\}\omega)\varphi(\{katika\}\omega\{kitabu\}\omega\{chao\}\omega)\varphi|\Phi$

(i) (Majibu yamo katika kitabu chao)

$|(\{Majibu\}\omega\{ya\}\omega\{katika\}\omega\{kitabu\}\omega\{chao\}\omega)\varphi|\Phi$

(ii) (Majibu yanayopatikana katika kitabu chao)

**Chanzo:** Uwandani (2022)

Mifano katika (6) hapo juu inaonesha kuwa kirai-fonolojia katika maana ya kwanza kinagawika baada ya ‘ya’ ya kitenzi kishirikishi ambapo mpaka wake katika matamshi unadhihirika waziwazi. Endapo hautawekwa hapo, mpaka huo utafutwa na kuwa katika kirai-fonolojia kinachofuata na kuleta maana ya (ii) ambayo ni tofauti na ile ya kwanza. Aidha, hadhi ya kipashio

husika hubadilika kisintaksia. Hivyo, utamkaji ni kipengele muhimu sana katika udhihirishaji wa tungo za kisintaksia na mipaka yake kulingana na maana inayokusudiwa. Maelezo haya huendana na mtazamo wa awali wa uhusiano wa fonolojia arudhi na sintaksia wa moja kwa moja (Hayes, 1989).

Sanjari na hayo, katika kujadili kuathiriana kwa fonolojia na sintaksia katika tungo, kuna maelezo yanayoonesha kuwa wakati fulani mipaka ya kifonolojia hutofautiana na mipaka ya kisintaksia. Mawazo haya hujitokeza katika lugha nyingi duniani (Grosjean na Gee, 1987). Hii ina maana kwamba, katika baadhi ya tungo vipashio vya muundo wa fonolojia arudhi hutofautiana na vipashio vya muundo wa kisintaksia. Tofauti hii, hususani katika tungo za Kiswahili imeleta changamoto kwa baadhi ya watumiaji, hasa katika uandishi. Katika uandishi, mara nyingi, mipaka mikubwa ya uarudhi hubainishwa na koma. Hivyo, watumiaji hao hujikuta wanaweka koma mahali pasipohitajika kisintaksia kwa kufuata mipaka ya vipashio vya kiarudhi. Mifano hapa chini kutokana na mahojiano na walimu na wanafunzi wa Kiswahili inadhihirisha hilo kama ilivyoielezwa katika utangulizi.

7. (a) \*Alisema kuwa, hawatarudia mchezo wao.

$$\begin{array}{l} |(\{Alisema\}\omega \quad \{kuwa\}\omega)\phi \quad (\{hawatarudia\}\omega \quad \{mchezo\}\omega \\ \{wao\}\omega)\phi | \Phi \text{ (F. Arudhi)} \\ ( \quad \quad \quad ) \text{ (Sintaksia)} \end{array}$$

(b) \*Tunahofu kwamba, yatatokea mabaya.

$$\begin{array}{l} |(\{Tunahofu\}\omega \quad \quad \quad \{kwamba\}\omega)\phi \quad \quad \quad (\{yatatokea\}\omega \\ \{mabaya\}\omega)\phi | \Phi \text{ (F. Arudhi) } \dots\dots\dots ) \quad \quad \quad \text{(Sintaksia)} \end{array}$$

**Chanzo:** Uwandani (2022)

Mifano katika 7 (a) na (b) inaonesha jinsi ambavyo baadhi ya watumiaji wa Kiswahili hujikuta wanatawaliwa na utamkaji katika kuandika miundo ya sintaksia ilhali miundo hiyo ni tofauti kimuundo na kiarudhi. Hali hii inawahimiza watumiaji kufahamu kuwa fonolojia na sintaksia huweza kuhusiana moja kwa moja au si moja kwa moja ingawa hutegemeana na kuathiriana katika kutoa ujumbe uliokusudiwa. Hali kama hii si ngeni katika

lugha za Afrika kama inavyodhihirishwa katika kazi ya Patin na Rialland (2006) na Downing (2011).

## 5.0 Hitimisho

Makala hii imekusudia kuonesha namna fonolojia na sintaksia huathiriana kiasi cha kubadilisha maana katika tungo. Ikiwa msemaji hatazingatia mipaka ya kiarudhi katika utamkaji wake, basi atajikuta anazalisha tungo zisizokubalika kisintaksia au zisizotoa maana inayoeleweka kwa wasikilizaji. Aidha, makala inaonesha kuwa kubadilisha utamkaji kwa kuhamisha mipaka ya muundo arudhi wa tungo huweza kubadilisha hadhi za vipashio vya kisintaksia na hata kubadili maana iliyokusudiwa na msemaji. Vilevile, upangiliaji tofauti wa vipashio vya kisintaksia na kusudio la msemaji huathiri utamkaji wa tungo kwa kusogeza au kuhamisha mipaka ya muundo arudhi katika tungo. Sanjari na hayo, ingawa ni kwa uchache, inaonesha kwamba watumiaji wasipokuwa makini katika kuangalia uhusiano wa fonolojia na sintaksia katika tungo, huweza kujikuta wanatawaliwa na utamkaji katika uandishi wao. Hivyo, sentensi zao zitakuwa na koma zisizohitajika kisintaksia kwani si lazima mipaka ya kirai-fonolojia au kirai-kiimbo ioane na ile ya kisintaksia kila wakati. Aidha, imebainika pia kuwa wakaa nao unahusika, kwa baadhi ya maneno ndani ya tungo, katika kufanya kazi pamoja na sintaksia kutoa maana ya tungo iliyokusudiwa.

## Marejeleo

Ackema, P. na Neeleman, A. (2004). *Beyond Morphology: Interface Conditions on Word Formation*. New York: Oxford University Press.

Büring, D. (2016). *Intonation and Meaning*. Oxford Scholarship Online.

Downing, L. J. (Mh.) (2011). *Questions in Bantu Languages: Prosodies and Positions*. ZASPiL 55.

- Downing, L. J. (2013). Issues in the Phonology-Syntax Interface in African Languages. Katika Orié, O. O. na Sanders, K. W. (Wah.) *Selected Proceedings of the 43rd Annual Conference on African Linguistics*. 26-38. Somerville, MA: Cascadilla Proceedings Project.
- Elfner, E. (2018). The Syntax-Prosody Interface: Current Theoretical Approaches and Outstanding Questions. Katika *Linguistics Vanguard*: De Gruyter
- Farmer, A. K. (1985). Modular Theories of Grammar. Katika *Annual Review of Anthropology*. Juz. 14. Kur. 25-48
- Grosjean, F. na Gee, J. P. (1987). Prosodic structure and spoken word recognition. Katika *Cognition*, Juz. 25: 135-155
- Hayes, B. (1989). Prosodic Hierarchy in Meter. Katika Kiparsky, P na Youmanns, G (wah.) *Rhythm and Meter*. 201-260. Academic Press, Inc.
- Mashauri, M. A. (2018). Mwingiliano wa Mashartizuizi ya Viwango vya Sarufi katika Uzalishaji wa Nomino Ambatani katika Kiswahili Sanifu. Tazmili ya Shahada ya Uzamivu katika Kiswahili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Nespor, M na Vogel, I. (1982). Prosodic domains of external sandhi rules. Katika H. Van der Hulst na Smith, N (wah.) *The structure of Phonological Representation (Part I)*. Dordrecht: Foris.
- Nespor, E. na Vogel, I. (1986). *Prosodic Phonology*. Dordrecht: Foris
- Patin, C. na Riailand, A. (2006). On the Nature of Rules Sensitive to Syntax: The case of Makonde Tonology. Katika *Prosody and Syntax - Cross-Linguistics Perspectives*. 285-302: John Benjamins Publishing Company.

Selkirk, E. O. (1978). On Prosodic Structure and Its Relation to Syntactic Structure. Katika Fretheim, T (mh) *Nordic Prosody*. Trondheim: Tapil, 1981. 111-140

Truckenbrodt, H. (1995) Phonological Phrases: Their Relation to Syntax, Focus, and Prominence. M.A Linguistics (Published). MIT. USA